

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA  
Simu Na: +255 26 2321607  
Nukushi: +255 26 2322116  
Barua pepe:[ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)  
Unapojibu tafadhali taja:-



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Mtaa wa TAMISEMI,  
S.L.P. 1923,  
41185 DODOMA.

Kumb. Na. EB.151/297/02/102

20 Januari, 2023

Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji,  
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya,  
**TANZANIA BARA.**


### **YAH: KUSAJILI WATUMIAJI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA KUTUMIA MAJINA NA TAARIFA ZAO HALISI**

Tafadhali, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imebaini kuwepo kwa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazosajili watumiaji wa mifumo ya TEHAMA kwa kutumia majina yasiyo halisi (**Generic User Names i.e Manager, Admin, Super User**).

2. Kuepuka kwenda kinyume na miongozo ya Serikali Mtandao, endelea kusimamia na kuhakikisha kwamba watumiaji wote wa mifumo wanasa jiliwa kwa kutumia majina na taarifa zao halisi za kiutumishi. Sambamba na hilo, akaunti zote zinazotumika kwenye mifumo zenye majina yasiyo halisi zisitishwe matumizi na zififishwe (**deactivated and disabled**) MARA MOJA. Pamoja na hivyo, watumiaji wa mfumo wakumbushwe kutochangia nywila (password sharing) wanazotumia kuingia kwenye mifumo.

3. Wote tunapaswa kuendelea kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi bora, sahihi na salama ya mifumo ya TEHAMA. Afisa TEHAMA na Mkaguzi wa Ndani wahakikishe haya yanazingatiwa na user matrix za mifumo inatumika ipasavyo. Suala hili litakaguliwa na Ofisi ya Mkoa, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali (IAG), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali (CAG), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, hivyo lichukuliwe kwa uzito unaostahili.

Ninawashukuru kwa ushirikiano wenu. **KAZI IENDELEE.**

  
Prof. Riziki S. Shemdoe  
**KATIBU MKUU**

Nakala:- Makatibu Tawala wa Mikoa  
**TANZANIA BARA.**

Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Serikali Mtandao - eGA,  
Mji wa Serikali - Mtumba,  
Mtaa wa Mtandao,  
S. L. P. 2833,  
**DODOMA.**